Umepokea Barua kuhusu Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE). Ni nini Kinachofuata?

Umepokea barua kutoka kwa wilaya ya shule kwa sababu familia yako inazungumza lugha nyingine isipokuwa Kiingereza nyumbani. Mtoto wako anaweza kustahiki Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE).

1

Wilaya ya shule hujaribu ujuzi wa mtoto wako wa lugha ya Kiingereza. Hii ni pamoja na:

- kusoma
- kuandika
- kusikiliza
- kuongea



Ikiwa mtoto wako anastahiki, wilaya ya shule itakutumia matokeo yake ya mtihani.

Pia watapendekeza mpango wa Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE) uwekwe shuleni.

2

Una chaguo. Jifunze kuhusu haki zako na chaguo zako.



Hivi ndivyo unavyoweza kufanya!

- Tembelea programu zinazopatikana.
- Hudhuria mikutano na makongamano kuhusu Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE).
- Chagua uwekaji tofauti unaopatikana.

3

Ikiwa mtoto wako yuko katika mpango wa Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE), shule itajaribu ujuzi wa mtoto wako wa Kiingereza mara kwa mara ili kuona kama yuko tayari kuondoka kwenye mpango huo.


Kama wanafunzi wenye mafanikio wa lugha nyingi, wanaweza kupata tuzo, Muhuri wa Serikali wa Kufahamu Lugha Mbili.

Wewe na shule ni washirika katika elimu ya mtoto wako.

Hebu tushirikiane ili kuongeza mafanikio ya mwanafunzi wako!

Hizi ni baadhi ya hatua zinazofuata:

- Wafahamu walimu na wafanyakazi
- Jifunze kuhusu Muhuri wa Serikali wa Kufahamu Lugha Mbili
- Uliza maswali na ushiriki habari
- Jihusishe na Baraza la Ushauri la Wazazi wa Wanafunzi wa Kiingereza (English Learner Parent Advisory Council, ELPAC)



Nyenzo hii iliundwa kwa ajili ya Idara ya Massachusetts ya Elimu ya Msingi na Sekondari na Kituo cha Ushirikiano cha Familia cha Jimbo Lote la Massachusetts, mpango wa Shirikisho la Watoto Wenye Mahitaji ya Pekee.

Je, una maswali? Wasiliana na shule yako: